
# MKRISTO KATIKA ULIMWENGU ULIOJAA ROHO



BIBLE STUDIES FOR AFRICAN YOUTH

# MKRISTO KATIKA ULIMWENGU ULIOJAA ROHO

Kimeandikwa na Paul Kyalimpa Amooti, Josphat M.M. Gikiri
na Andrew Mwenge

**BIBLE STUDIES FOR AFRICAN YOUTH**

Africa Coordinated Curriculum
for Bible Study

Y1-4PS

Used with permission of International Publications Services

Published by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI

©Copyright, 1990
Baptist Publications House
All Rights Reserved

2. Je! unamtegemea Roho Mtakatifu kukuongoza katika maombi na kusoma Biblia? Mwombe akufundishe kila wakati unaposoma Neno la Mungu.

3. Kumbuka kila wakati kwamba una adui ambaye ni Shetani. Mtegemee Roho Mtakatifu kukusaidia. Kumbuka maneno ya 1 Yohana 4:4.

unapookoka. Roho huufanya umoja huu kuwepo maishani mwako. Roho hukuongoza kuwa mmoja na Mungu.

3. Roho Mtakatifu hukufanya umtii Mungu. Kuna wimbo unaoelezea yale ambayo Roho hufanya maishani mwetu. Unasema, nitapenda Roho anaponiambia kupenda na kutii Roho wa Bwana. Nitakiri dhambi zangu, nitaomba, nitashuhudia, nitajifunza Neno la Mungu, nitawasamehe wengine na nitafanya kila jambo Roho anaponiambia. Mwamini anatakiwa kutii hivyo. Itadhihirisha kwamba unampenda Yesu. Utamwona na kumjua Yesu unapoendelea kumtii.

4. Roho hukuongoza kuomba na kusoma Biblia. Hukuwezesha kushiriki na Mungu. Ni lazima Mungu awe wa kwanza maishani mwako. Unapaswa kupanga wakati wa kushiriki naye kila siku. Endelea siku nzima katika ushirika huo. Zaburi 88:13 inasema, "...Na asubuhi maombi yangu yatakuwasilia."

5. Biblia inasema pia kwamba Neno la Mungu lisiondoke kinywani mwako. (Yoshua 1:8) Unapaswa kulipenda na kulitafakari kila wakati. Biblia ni Neno la Mungu uliloandikiwa. Mungu hunena nawe kupitia kwa Biblia. Roho hukufundisha unapolisoma. Kwa hivyo, mtegemee. Roho unaposoma Biblia.

6. Roho hukuongoza kupigana vita na Shetani. Shetani atakujaribu. Hata atakuletea mateso, lakini Roho yu pamoja nawe. Mwombe na akusaidie.

**KAZI YA KUFANYA**

1. Je! maisha yako yanabadilika na kuwa kama ya Yesu? Je! umejifunza nini katika kitabu hiki ambacho kitakusaidia kujua kwamba maisha yako yatabadilika?



# YALIYOMO


| SURA | UKURASA |
|---|---|
| 1. Shetani, Mwanzo na Kuanguka Kwake | 5 |
| 2. Shetani, Kazi Yake Siku Hizi | 10 |
| 3. Shetani na Hukumu | 14 |
| 4. Uchawi na Kazi ya Shetani | 18 |
| 5. Jinsi ya Kutambua Uchawi | 21 |
| 6. Uchawi na Mkristo | 26 |
| 7. Roho Mtakatifu na Utatu | 29 |
| 8. Roho Mtakatifu na Uongozi | 34 |
| 9. Kuja kwa Roho Mtakatifu | 38 |
| 10. Kazi ya Roho Mtakatifu | 41 |
| 11. Kujazwa na Roho Mtakatifu | 45 |
| 12. Roho Alifanyika Mwili | 50 |
| 13. Kuongozwa na Roho Mtakatifu | 54 |

# KUHUSU WAANDISHI

Kitabu hiki kimeandikwa na Paul Kyalimpa Amooti, Josphat M.M. Gikiri na Andrew Mwenje. Walitumia kitabu cha International Publications Services chenye kichwa hiki kama msaada wa kuandika upya katika mtindo mpya.

Amooti ni mwinjilist huko Uganda. Ametumika kama mkurugenzi wa Bible Way Correspondence School katika nchi yake. Yeye ni mshiriki wa Kampala Baptist Church.

Gikiri ni mwalimu huko Maragua, Kenya. Yeye ni mshiriki wa Kaimiri Baptist Church, na anatoka Kenya.

Mwenge ni mchungaji wa vijana wa Kampala Baptist church ambako ni mshiriki.

Roho Mtakatifu humwongoza Mkristo kuishi maisha ya ushindi. Yesu alikuwa na lengo alipoishi duniani. Lengo lake lilikuwa kumtii Baba yake. Lengo lake ndilo lililomfanya Yesu na watawala wa ulimwengu wasipatane, lakini Yesu alikuwa na nguvu kushinda shetani. Hakutenda kulingana na majaribu yake. Yesu alimshinda kabisa Shetani alipoangikwa msalabani. Mkristo ye yote anaweza kushinda Shetani siku hizi kwa kufuata uongozi wa Roho Mtakatifu.

Kila Mkristo anapaswa kujua kwamba yule aliyoko ndani yake ni Mkuu ibilisi, na Shetani alishindwa msalabani. Shetani hawezi kamwe kumshinda Mungu.

**MAFUNZO YA SURA HII KWANGU**

**Je! ni lini ambapo Roho wa Mungu hutuweka huru kutoka kwa dhambi na mauti?**

Yesu alimwita Roho Mtakatifu Mshauri. Alikuja maishani mwako ili akusaidie. Yohana ametaja sehemu sita ambazo Roho Mtakatifu hukuongoza. Roho hutumia sehemu hizi sita kukuweka huru kutoka kwa dhambi na mauti.

1. Roho Mtakatifu hukuweka huru kutoka kwa maisha ya tamaa za mwili. Hukuweka huru kutoka kwa dhambi. Hukuongoza kuupata uzima wa milele. Maisha ya uzima wa milele ni ya Mungu, kwa hivyo Roho hukuongoza katika maisha ya Mungu.

Hutapenda dhambi ukiwa katika maisha haya. Roho Mtakatifu hubadili maisha yako uwe kama Kristo. (Warumi 8:29) Maisha yako huwa matakatifu, safi, yenye furaha na upendo. Wewe huwa kama Yesu.

2. Roho Mtakatifu hukuongoza katika maisha ya kuwa mmoja na Mungu. Huwa unaunganishwa na Mungu katika Kristo

hutuongoza. "...Mimi ni ndani ya Baba yangu, nanyi ndani yangu, nami ndani yenu" (kifungu cha 20).

Yesu aliwaonyesha wanafunzi wake umoja wa ajabu kati ya Mungu na waamini kupitia kwake. Mtu hupokea Roho Mtakatifu anapomkumbali Yesu Kristo maishani mwake. Roho humsaidia kuelewa umoja huu. Tunajifunza katika Yohana 14:21-24 kwamba ushirika wetu na Kristo hutegemea upendo. Utii huleta upendo, na upendo huleta utii. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba ni lazima wamtii kama Bwana wa maisha yao baada ya kumpokea. Hii itaonyesha tunda la roho ambalo ni upendo.

Yesu aliwaahidi waamini ufunuo wa Mungu. Roho Mtakatifu huendelea kutuonyesha mengi kuhusu Mungu tunapomtii.

Yesu aliwatokezea wale waliompenda baada ya kufufuka. Hakuwatokezea Waandishi na Mafarisayo wala Wayahudi waliomkataa.

Vifungu vya 25-27 vinatuonyesha kwamba Roho Mtakatifu huendelea kutufundisha. Hutufafanulia mafundisho ya Kristo na kutupa amani yake. Yesu aliahidi wafuasi kwamba Roho atakuwa mwalimu wao. Roho angewaongoza kuelewa Neno la Mungu. Angewaongoza waishi maisha matakatifu. Siku hizi, Roho huwafundisha watu wote wanaomjua Yesu kuwa Bwana. Humwongoza Mkristo huyo kwa ukweli mkuu wa Mungu. Mkristo ni mwanafunzi katika ufalme wa Mungu.

Yesu aliwaahidi waanfunzi wake amani yake, wala si ya ulimwengu. (kifungu cha 27) Hii ni amani ya milele, amani ya ushindi. Mwamini hapaswi kuogopa amteso. Anapaswa awe tayari kukabiliana na hali yo yote akiwa na matumaini ya kushinda. Roho hutuongoza kuelewa amani hii ya ajabu. Ni yetu wakati wa mateso. Hutuletea ushindi. Mungu hufanya mambo yote kutuletea mema. (Warumi 8:28)



SURA YA KWANZA

# SHETANI, MWANZO NA KUANGUKA KWAKE

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza asili ya Shetani na jinsi alivyokuwa adui.

SOMO KUTOKA: Ezekieli 28:12-18, Isaya 14:12-14, Mwanzo 3

VIFUNGU VYA LEO: Ezekiel 28:12-18, Isaya 14:12-14

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:"Usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema" (Warumi 12:21).

## KUSOMA SOMO

## UTANGULIZI

Kuna hadithi inayohusu mchungaji maarufu sana na pia tajiri. Alirithi pesa na mali baba yake alipokufa. Alitoa mali kwa ujenzi wa kanisa na kuwasaidia watu wenye mahitaji. Aliwashauri waliohitaji mashauri. Alikuwa mtu mashuhuri sana katika kijiji hicho.

Hata hivyo, mchungaji huyu maarufu alianguka siku moja. Alipoteza mamlaka yake, cheo, mali na marafiki. Mwishowe hakuwa na cho chote. Alipoteza kazi, huduma yake ikaisha, jamaa yake wakamwacha na akawa maskini.

Je! shida ilikuwa nini katika maisha ya mchungaji huyu? Je! kwa nini alipoteza kila kitu? Jambo moja lilifanyika maishani mwake. Alianza kujivuna na kutaka aongoze kila kitu.

Maisha ya mchungaji huyu ni kama ya Shetani. Shetani alikuwa malaika wa Mungu, lakini alianguka kabisa. Hebu tujifunze asili ya Shetani na jinsi alivyopata kuwa adui.

## MAELEZO

Soma Ezekieli 28:12-18. Huu ni uwakili juu ya mfalme mwenye hekima wa Tiro. Mfalme alikuwa tajiri, mwenye mali nyingi, lakini alianza kujivunia mali na hekima yake. Alijidai kuwa Mungu, na huu ukawa mwanzo wa mwisho wake. Mfanya alifanya dhambi kwa kujivuna na kudai kuwa Mungu, na Mungu akamwadhibu.

Hebu tuangalie matendo ya mfalme wa Tiro na tujifunze asili ya Shetani. Maandiko haya yanatuonyesha tabia, mahali na cheo cha Shetani kabla ya kufukuzwa kutoka mbinguni.

Kifungu cha 12 kinaelezea tabia yake alikuwa kiumbe mkamilifu kabla ya kuanguka. Alishirikiana vizuri na Mungu, pamoja na malaika wengine. Alijaa wema na hekima. Hapakuwa malaika mwingine mbinguni kama yeye. Alikuwa mwema kwa wote.

Vifungu vya 13 na 14 vinatuonyesha mahali alipokuwa. Alikwenda katika bustani ya Edeni, bustani ya Mungu. Shetani alikuwa malaika mwenye uwezo. Alipaswa kumwabudu Mungu na kumtumikia kama malaika wengine. Alipaswa kumtii Mungu. Alipewa mamlaka juu ya malaika wengine. Alilindwa na malaika wengine. Alikuwa karibu na Mungu na mjumbe wa Mungu. Aliwakilisha malaika wengine. Kwa hivyo alikuwa na cheo kikubwa.

Soma vifungu vya 15-16 kuona dhambi yake. Shetani alifanya maovu mbele za Mungu. Alianza kujivunia ukamilifu wake, hekima, uzuri, cheo na makao yake. Majivuno yalikuwa dhambi mbele za Mungu. Alitamani kuwa kama Mungu.

Vifungu vya 12-18 vinatwambia adhabu yake Shetani alifukuzwa mbinguni kwa sababu ya maovu yake. Alipoteza kila kitu. Majivuno ndiyo chanzo cha kuanguka kwake, na akatupwa jehanum.



Chuma hicho hakijabadilika kamwe. Sheria ya uzito wa kuzama ingali vile vile, lakini sasa imepingwa na sheria nyingine, sheria ambayo huhusu vifaa vinavyoelea. Sheria hii imeitoa chuma kwenye sheria inayohusu uzito wa kuzama.

Sheria hizi mbili, ya uzito wa kuzama na vifaa vinavyoelea ni kama nguvu aina mbili. Ni kama nguvu za Shetani na nguvu za Roho Mtakatifu.

Sisi huwa chini ya sheria ya dhambi na mauti kabla ya kumpokea Kristo. Kisha Roho huanza kutawala tunapompokea Yesu kuwa Mwokozi. Sheria ya dhambi na mauti huwa imeshindwa. Huwa haina nguvu tena. Huwa huru nayo. Roho wa Mungu huanza kutawala. Yesu hututoa mautini na kutupa uzima. Nguvu zake huwa kuu kuliko za mauti. (1 Yohana 4:4) Tutajifunza leo jinsi tunavyoongozwa na Roho Mtakatifu.

## MAELEZO

Soma Yohana 14:16-31. Neno la Kiyunani lililotumiwa katika kifungu cha 16 kama msaidizi, linamaanisha pia Roho, mtu aliyeitwa. Roho ni mtu aliyeitwa kusaidia. Huja kusaidia kwa njia tofauti kwa mfano, kuishi, kushauri, kutia moyo, kufariji, kuongoza na kufundisha.

Tunasoma katika vifungu vya 18-20 kwamba Roho huleta uzima (Matendo 2:33) na humwunganisha mwamini na Mungu.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake katika kifungu cha 19, "...Na kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai." Maisha yake yalipaswa kuwa maisha yao. Walipaswa kuishi kama Kristo. Maisha haya ni ya uzima wa milele. Hayana mwisho na yanampendeza Mungu. Haya ndiyo maisha tunayopata tunapompokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wetu. Roho

Mwamini Mungu kwa sababu atafanya jinsi anavyosema. Atatimiza ahadi zake kama utamtii. Hatakosa kamwe.

**KAZI YA KUFANYA**

1. Mshukuru Mungu kwa kumtuma Yesu ulimwenguni.

2. Andika orodha ya faida utakayopata maishani kwa kumjua Yesu. Iweke katika Biblia yako ili uweze kuongezea unapopata jambo jipya.

3. Mwonyeshe rafiki yako orodha hiyo na mzungumzie pamoja.

## SURA YA KUMI NA TATU

# KUONGOZWA NA ROHO MTAKATIFU

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza jinsi kuongozwa na Roho Mtakatifu.

SOMO KUTOKA: Yohana 14:16-31

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 14:16-31

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa" (Yohana 15:7).

**KUSOMA SOMO**

**UTANGULIZI**

Je! ni nini hufanyika wakati chuma ulichoshika mkononi kinapoponyoka ukiwa umesimama kando ya ziwa la maji? Huanguka majini na kuzama. Hili ni thibitisho la uzito wa chuma hicho. Lakini chuma hicho kikifungiwa kwenye mbao halafu kitoswe majini, kitaelea. Je! kwa nini?



Fungueni katika Isaya 14:12-14. Nyota ya alfajiri, iliyoko katika kifungu cha 12 ni Shetani. Shetani alianguka kutoka mbinguni. Yesu amesema katika Luka 10:18, "...Nilimwona Shetani, akianguka kutoka mbinguni kama umeme."

Kuna tamaa aina tano zilizosababisha kuanguka kwa Shetani. Ziko katika Isaya 14:13-14: Alitamani kupanda "...mpaka mbinguni...." Alitaka kupanda mpaka mbingu za juu. Alitamani kukiinua "...kiti changu juu..." Alitaka kuwa juu ya nyota za Mungu. Alitaka ufalme wake uwe juu ya muumbo wa Mungu. Alitamani kuketi "...juu ya mlima wa mkutano...." Shetani alitaka kukalia ufalme kama Mungu. Alitamani kupaa "...kupita vimo vya mawingu...." Alitaka Mungu awe chini yake. Mwishowe alitamani kufanana "...na yeye Aliye juu." Alitaka kuwa kama Mwenyezi Mungu.

Tamaa hizi zote zinaonyesha majivuno. Majivuno ni dhambi. Shetani alifanya dhambi mbele za Mungu na mbele za viumbe vya Mungu. Hii ndiyo sababu alianguka hadi kiwango cha mwisho.

**MAFUNZO YA SURA HII KWANGU**

Asili na kuanguka kwa Shetani kunatufundisha tusiwe kama yeye. Shetani aliishi maisha kamilifu hapo mwanzo. Maneno, mawazo na matendo yake yalikuwa kamilifu na yenye haki. Ushirika wake na Mungu ulikuwa kamilifu. Hata hivyo, mambo yalibadilika. Alikosa ukamilifu wake. Alianza kujivuna, baba mwenye uongo wote. Ukawa mwisho wa ushirika wake na Mungu.

Je! tendo hili linatufundisha nini? Linatufundisha kwamba Shetani ni mfano mbaya. Ni adui wetu kwa yale aliyofanya kukosa ukamilifu. Tusifuate mfano wake na kuanza kujivuna. Hiyo ni dhambi, na dhambi huzuia ushirika wetu na Mungu.

Tunaona pia kwamba Shetani alikuwa na hekima. Alikuwa na hekima ya Mungu. Lakini alitumia vibaya hekima hiyo. Alitaka kuwa juu ya Mungu. Alifikiri kwamba wengine wapo kumtumikia. Alidai kuwa Mungu. Huu ndio mwanzo wa majivuno na kuanguka kwake. Hatupaswi kufuata mfano wa Shetani. Bali tunapaswa kufuata mfano wa Kristo aliyejitoa kuwa mtumishi. Kristo alikuja kutumika bali si kutumikiwa.

Tumeona kwamba Shetani aliishi maisha makamilifu mbinguni. Alipewa wajibu mkuu. Malaika wengine walikuwa chini yake, lakini alianza kufanya maovu. Dhambi iliingia maishani mwake. Alianza kujivuna alipotambua kwamba anapendwa. Alijivunia kazi na matendo yake. Alisahau neema ya Mungu iliyomwezesha kufika pale alipo. Alifikiri kwamba Mungu alimkubali kwa sababu ya hekima yake, matendo na kazi nzuri. Alikuwa kipofu na kutoona kwamba neema ilitosha kumfanya apendwe na kukubaliwa na Mungu. Shetani ni mfano mbaya!

Hatupaswi kujivunia kazi na matendo yetu. Biblia inasema, "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu" (Waefeso 2:8-9). Kazi nzuri, kama kwenda kanisani kila Jumapili, kutoa pesa kanisani, kuwasaidia maskini na kuomba hazitufanyi tukubaliwe na Mungu. Matendo mazuri hayamwokoi mtu. Yesu ndiye hutufanya tukubaliwe na Mungu. Yesu anaokoa. Mtu anayeokolewa na Yesu huwa mtumishi na si bwana mkubwa. Huwa mtumishi wa Mungu na watu wengine. Hujiona kwamba anatumiwa na Mungu kuhudumu. Yeye ni chombo cha Mungu. Wakristo wanapaswa kuwa na tabia hii.

Tuliona kwamba Shetani alikuwa na cheo mbinguni. Alimfuatia Mungu. Lakini hakutosheka na cheo wala mamlaka yake. Alijaribu kujilinganisha na Mungu. Huu ni mfano mwingine mbaya wa Shetani. Ni lazima tutosheke na



Biblia inasema kwamba Mungu anataka kila mtu aokoke na ajue ukweli. "Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi" (Yohana 14:6). Mungu alimtuma Yesu kuja ulimwenguni akuokoe kutoka dhambini. Anataka ujue njia ya kupata uzima wa milele. Huwa unamjua Mungu unapomjua Yesu.

Yesu akasema, "...Aliyeniona mimi amemwona Baba;..." (Yohana 14:9). Huwa unamfahamu Mungu uwapo ndani ya Yesu. Unaweza kujua mapenzi yake kwa maisha yako, upendo wake na asili yake. Haya ndiyo Mungu anataka ujue na uwe nayo.

Hata hivyo, watu hawajui mapenzi na upendo wa Mungu. Hawajampokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wao. Wamesikia habari zake. Lakini hawajawahi kumpokea. Wanaweza kufahamu mapenzi na upendo wa Mungu kama watampokea Yesu awe Mwokozi.

Mtu hupokea uzima wa milele anapomkubali Yesu. Biblia inasema, "Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele..." (1 Yohana 5:13). Mungu anataka ujue kwamba una uzima wa milele unapozaliwa katika Roho, yaani unapompokea Yesu kuwa Mwokozi wako. (Yohana 3:3-6)

Biblia inasema, "Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu" (Waefeso 1:13). Roho ndiye ishara ya Mungu kwamba u mali yake. Roho huyu ndiye anayekuongoza kwa katika maisha mapya unayopokea. Soma Yohana 16:13.

Yesu anapaswa kuwa mfano wako unapoishi maisha mapya. Amejaribiwa jinsi tunavyojaribiwa, lakini yeye hakufanya dhambi. Soma 1 Wakorintho 10:13. Atakusaidia kushinda majaribu.

"Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake..." (kifungu cha 14). Neno lilifanyika mwanadamu. Soma Luka 2:1-7 na vifungu vya 21 na 52.

Hata ingawa Yesu alizaliwa kama watu wengine, kuzaliwa na maisha yake yalikuwa mfano wa ajabu. Roho Mtakatifu alihusika katika kuzaliwa kwake. Yeye ni Mungu pamoja nasi. Hii ni kwa sababu Baba na Roho walikuwa pamoja naye. Yeye kama mtu, alikuwa na mwili wa kibinadamu wenye udhaifu wote. Kwa hivyo alikuwa mwanadamu. Yesu alilia machozi, alichoka na alisikia njaa. Lakini hakufanya dhambi hata ingawa alijaribiwa.

Soma Wafilipi 2:5-8. Yesu "...alikuwa yuna namba ya Mungu..." (kifungu cha 6). Kabla ya kufanyika mtu neno ya Kiyunani, namna, lililotumiwa hapa linamaanisha kitu kisichobadilika. Kwa hivyo, Yesu hakubadili asili yake ya Mungu. Alikuwa Mungu hata alipofanyika mwanadamu. Mwana alikuwa na Baba kutoka milele. Walikuwa na utukufu sawa na maumbile. Hata hivyo, tunaambiwa kwamba Yesu alivua utukufu wake, lakini akabaki na maumbile au hali sawa na Baba. Utukufu wa nje wa Yesu ulibadilika alipofanyika mtu. Paulo alisema Yesu, "...alijifanya kuwa hana utukufu, akatwa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu" (kifungu cha 7). Hakushikilia cheo chake jinsi alivyostahili. Bali alikiacha. Mungu alimwinua kwa kufanya hivyo. Soma Wafilipi 2:9-11.

Mungu alimwinuaje Yesu? Kwanza alimpa jina ambalo lashinda majina yote. Pili, kila goti litapigwa mbele ya jina lake. Yesu akawaambia,"Kwa maana kitu ajikwezaye atadhiliwa, naye ajidhiliye atakwezwa" (Luka 14:11).

**MAFUNZO YA SURA HII KWANGU**

Je! kwa nini Mungu alimtuma Mwokozi ulimwenguni? Je! hiyo inakuhusu nini?



kile tulicho nacho. Je! umewahi kujaribiwa kutaka mali ya mwenzako? Watu wengine huiba mali ya wenzao. Sisi huwa kama Shetani tunavyofanya hivyo. Hutenda dhambi. Matokeo ya dhambi isiyosamehewa ni kutupwa jehanum. Kumbuka kwamba Shetani ni adui yetu. Hutujaribu tumfuate. Alimjaribu Hawa. (Mwanzo 3) Alimjaribu Yesu. (Mathayo 4) Alitaka Yesu amfuate.

Shetani bado anawajaribu watu siku hizi. Jihadharini naye. Mpinge anapokujia. Kumbuka kwamba, "Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili" (1 Wakorintho 10:13).

Chagua leo! Je! utafuata majaribu ya Shetani, au utafuata maagizo ya Bwana?

**KAZI YA KUFANYA**

1. Jifunze jinsi Shetani alivyomjaribu Hawa katika Mwanzo 3, Yesu katika Mathayo 4 na watu wengine katika Agano Jipya.

2. Chunguza maisha yako na uone wakati ambapo Shetani amekujaribu. Ulifanya dhambi ama ulifuata mfano wake. Mwombe Mungu msamaha wa dhambi hiyo.

3. Kumbuka kwamba majaribu si dhambi. Huwa dhambi unapomtii Shetani. Jaribu kukumbuka wakati ambapo huwa unajaribiwa. Je! ni mara ngapi ambapo huanguka, na ni mara ngapi humshinda Shetani?

4. Mwombe Mungu kila siku akusaidie kushinda majaribu.

## SURA YA PILI

# SHETANI, KAZI YAKE SIKU HIZI

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza yale ambayo Shetani anafanya ulimwenguni.

SOMO KUTOKA: Zakaria 3:1; Mwanzo 3:1-7; Ayubu 1:9; Mathayo 13:19; 4:3; Luka 11:14-26

VIFUNGU VYA LEO: Zakaria 3:1; Mwanzo 3:1-7; Ayubu 1:9; Mathayo 13:19; 4:3; Luka 11:14-26

KIFUNGU CHA KUKUMKBUKA: "Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze" (1 Petro 5:8).

**KUSOMA SOMO**

**UTANGULIZI**

Watu wengi hupenda kufuga mbwa. Wengine huwatumia kulinda nyumba zao. Wengine huwafuga kama rafiki. Kila mbwa hupewa jina, ili watu wamwite kwa jina lake.

Watu hufunga mbwa zao wakati wa mchana na kuwafungulia wakati wa usiku. Mbwa akiwa amefungwa hubweka tu anapowaona watu. Hawezi kuwadhuru. Hawezi kwenda mbali kwa sababu amefungwa. Lakini anaweza kumwuma mtu anapoikaribia na kuichezea. Wakati huu ndipo anapoweza kumfikia mtu huyo.

Shetani ni kama mbwa aliyefungwa. Anayo majina mengine. Alifungwa na Kristo na bado amefungwa hata sasa. Ananguruma kama simba aliyefungwa. Anafanya kazi akiwa amefungwa, lakini kazi yake ni ya muda tu. Hujaribu kuwadhuru watu, lakini ushindi wake unategemea udhaifu wa



moja yenye sehemu mbili tofauti. Sehemu hizi mbili haziwezi kutenganishwa kwa zote ni kitu kimoja.

Yesu, kama shilingi, anasehemu mbili tofauti. Yeye ni Mungu na pia mwanadamu. Kuzaliwa kwa Yesu na bikira kulikuwa mwujiza uliokuwa na utu aina mbili. Yesu alikuwa Mwana wa Mungu na Mariamu. Tutajifunza mengi kuhusu Yesu tunaposoma somo hili.

**MAELEZO**

Soma Yohana 1:1-3, 14. Neno la Mungu lilikuwepo ulimwengu ulipoaanza. Ni muhimu kujua kwamba Neno ambalo Yohana anazungumzia ni Yesu, Mwana wa Mungu. Je! Yohana alimaanisha nini kwa kumwita Neno? Akasema, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno...." Yohana alifikiria juu ya Mwanzo 1:1, "Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nini." Yohana alimaanisha kwamba Neno halikuumbwa. Neno lilikuwepo kabla ya uumbaji. Yesu alikuwepo kabla uumbaji wote.

Aliendelea kusema, "...naye Neno alikuwako kwa Mungu...." Je! Yohana alimaanisha nini? Yohana alikuwa akionyesha uhusiano kati ya Neno la Mungu. Yesu tu ndiye anayeweza kutuambia jinsi Mungu alivyo. Mapenzi ya Mungu kwetu, na jinsi upendo, moyo na mawazo ya Mungu yalivyo.

Kisha akasema, "...naye Neno alikuwa Mungu." Yohana hakuwa akisema kwamba Yesu anafanana na Mungu. Alikuwa anasema kwamba Yesu ni Mungu. Neno, Yesu, lilishiriki katika uumbaji. Kifungu cha 3 kinasema, "Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika." Neno, Yesu ni uzima na nuru ya wanadamu. Kifungu cha 4 kinasema, "Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu."

## KAZI YA KUFANYA

1. Mshukuru Mungu kwa Roho Mtakatifu wake anayeishi mioyoni mwa waamini.

2. Je! maisha yako yanabadilika na kuwa kama Kristo? Je! somo hili limetufundisha kwamba ni nini kinaweza kuleta mabadiliko haya?

3. Je! ni nini karama yako ya Kiroho? Waambie Wakristo wengine wakusaidie kuitambua kama huijui. Itumie kwa utukufu wa Mungu na kwa manufua ya wengine.

4. Mwombe Roho Mtakatifu akujaze kila siku. Ishi siku hiyo kwa ahadi iliyoko katika Wafilipi 4:13.

## SURA YA KUMI NA MBILI

# ROHO ALIFANYIKA MWILI

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba Yesu ni Mungu na pia mwanadamu.

SOMO KUTOKA: Luka 2; Yohana 1:1-14; Wafilipi 2:5-11

VIFUNGU VYA LEO: Luka 2; Yohana 1:1-14; Wafilipi 2:5-II

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake..." (Yohana 1:14).

## KUSOMA SOMO

## UTANGULIZI

Je! huwa unaona nini unaposhika shilingi mkononi mwako? Hebu geuza shilingi hiyo. Kila upande ni tofauti. Je! hii inamaanisha kwamba una shilingi mbili? La hasha! Ni shilingi



mtu huyo. Hawezi kumfikia mtu mpaka mtu huyo anapomwendea.

## MAELEZO

Shetani ana majina mengi katika Biblia. Yote yanaelezea kazi yake. Huitwa Shetani, nyoka, Ibilisi, mwovu, Beelzebul, mshawishi, mwongo na mengine mengi.

Hebu tuangalie jina lake, mshitaki. Kazi ya Shetani ni kuwashitaki watu. Alimshitaki Yoshua katika Zekaria 3:1. Yoshua aliwakilisha taifa la Israeli, watu wa Mungu. Shetani alimshitaki Ayubu mbele za Mungu katika Ayubu l:9; 2:4. Mashitaki yake yalileta vita vya kiroho kati ya neema ya Mungu na haki ya Ayubu. Lakini Shetani alishindwa. Katika Ufunuo 12:10, Shetani ni "...mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku."

Anaitwa pia mdanganyaji. Katika Mwanzo 3:1-7, Shetani alimdanganya Hawa na akamfanya ashuku neno la Mungu. Shetani hajaacha kudanganya. Yeye ndiye "...audanganyaye ulimwengu wote;..." (Ufunuo 12:9). Wakristo wanapaswa kujihadhari na kutodharau "... hila za Shetani" (Waefeso 6:11).

Shetani ameitwa mjaribu katika Mathayo 4:3. Alimjaribu Yesu. Shetani huwajaribu wanadamu wote kwa kuwashawishi wafanye dhambi. Alimjaribu Hawa, taifa la Israeli na Yesu. Huwajaribu watu Wakristo leo.

Shetani ameitwa pia mwovu. Yesu alimwita mwovu katika Mathayo 13:l9. Shetani hutaka kuwapotosha watu, jinsi yeye alivyompotovu. Yesu aliwaombea waamini wote walindwe kutoka kwa yule mwovu. (Yohana 12:15) Uwezo wa Shetani umeuzingira ulimwengu wote. (1 Yohana 5:l9)

Shetani ameitwa Beelzebul, mfalme wa pepo. (Luka 11:14-26) Jina hili linamwonyesha Shetani kuwa mtawala. Ni mtawala wa

mapepo. Hutawala pia mioyo ya watu ambao hawajaokoka. (Waefeso 2:2)

Jina hili, Shetani, linamaanisha adui au mshindani. Yeye humpinga Mungu na watu wa Mungu. Kusudi lake ni kuanzisha ufalme wa kumpinga Mungu.

## MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Shetani huwazuia watu ambao hawajaokolewa kukubali ukweli. Tunaambiwa katika Mathayo 13:19 kwamba hulinyakua Neno la Mungu kutoka kwa wale wanaosikia. Huwazuia wasiookoka kuelewa habari njema. Hujaribu kuwazuia wasiokoke. Pia, huwafunga wasiookoka ili wasiweze kutambua dhambi zao, wala haki na hukumu ya Mungu. Huzuia uwezo wa Roho Mtakatifu kumwongoa mtu ambaye hajaokoka. (Yohana 16:7-11)

Shetani humweka mwenye dhambi katika dini isiyo ya kweli. Humfanya mwanadamu kushuku wokovu wake. Huwafanya wafikiri kwamba wokovu huletwa na matendo mema, wala siyo neema. (Waefeso 2:8-9) Shetani huwafanya watu wengine waamini kwamba hakuna wokovu katika Yesu Kristo. Shetani huwafanya wasiookoka kuwachekelea waliookoka.

Shetani huwafanya wenye dhambi kuishi maisha maovu. Huwapa moyo wa kutamani kila kitu. Huwafanya watu wengine kuwa wachoyo. Huwapa wengine tamaa ya mali, na kuwatesa maskini.

Shetani huwashitaki Wakristo mbele za Mungu jinsi alivyomshitaki Ayubu. (Ufunuo 12:10) Huwadanganya Wakristo na kuwafanya wamshuku Mungu. Shetani huwafanya Wakristo washuku Neno la Mungu, uwezo na wema wake. Huwa anatumia maarifa sawa na yale aliotumia katika Mwanzo 1:3-7. Huwajaribu wasiookoka kufanya dhambi.



kazi aliyowapatia. Huwapa Roho huyo jinsi wanavyohitaji. Mkristo anaweza kujazwa na Roho mara nyingi.

## MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Kujazwa na Roho ni jambo linaloendelea kufanyika maishani mwa Mkristo. Hufanyika mara ya kwanza anapompokea Yesu kuwa Mwokozi. Hatungepata wokovu bila ya Roho wa Mungu. Ikiwa umempokea Yesu kuwa Mwokozi, unapaswa kufuata maagizo ya kujazwa Roho yaliyoko katika Yohana 7:37-39. Unapaswa kujua kwamba Roho anatawala na anaongoza maisha yako.

Je! huwa anaongoza maisha yako unapokiri dhambi zako? Je! hukusaidia kuishi maisha matakatifu? Au Je! unaishi maisha ya tamaa za mwili? Maisha ya tamaa za mwili hudhihirishwa na majivuno, hasira, maovu, uasherati, wizi na uzinzi. Lakini utatawaliwa na kuongozwa na Roho kama utatimiza masharti ya kujazwa Roho.

Je! utajuaje umejazwa na Roho? Ni rahisi sana kujua. Wakristo wengi hupata upendo wa kusema habari za Kristo kwa ujasiri. Hii ni sababu ya utimilifu wa Roho. Roho humfanya mtu akiri anapofanya dhambi. Soma Warumi 10:9-10.

Maisha yako hubadilika kwa sababu ya utimilifu wa Roho. "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! yamekuwa mapya" (2 Wakorintho 5:17). Maisha yako hubadilika jinsi unavyojazwa na Roho. Hatimaye huanza kuzaa matunda ya Roho yalioko katika Wagalatia 5:19-23.

Mwishowe, jinsi unavyojazwa na Roho, ndivyo utatumia karama za kiroho ziletwazo na Roho Mtakatifu.

5:22-23. Matendo ya waliojazwa na Roho ni tofauti na matendo ya kimwili. Roho aliwauliza Wagalatia kama walipokea Roho kwa kutii sheria au kwa imani. (Wagalatia 3:2-3) Walipokea Roho kwa imani. Hivyo ndivyo walivyopaswa kujazwa na Roho. Angewasaidia kuzaa matunda. Roho ndiye chanzo cha matunda yanayopatikana katika maisha ya Mkristo. Lakini mwanadamu ndiye chanzo kuzaa matunda maishani mwake kama anataka haki kwa kutii sheria. Hilo si tunda jema.

Yesu alisema kwamba mtu anapaswa kumpenda Mungu na jirani yake. Wakristo wengi huona hofu kwa sababu hawatii amri hii. Hawajatambua kwamba upendo ni tunda la roho. Si jambo linaloletwa na juhudi zao. Mungu ni pendo na Roho wake ni pendo katika moyo wa mwamini. Mwamini anapaswa kuwa na tunda la roho ambalo ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, wema, uaminifu, ustahimilivu na kiasi. Matunda haya yataonyesha kwamba amejazwa na Roho Mtakatifu.

Mtu anapojazwa na Roho huwa huru kutoka kwa hofu na woga. Huwaambia wengine habari za Kristo. Haionei haya injili au ndugu zake waliookoka. Soma 2 Timotheo 1:7-9 na Matendo 9:27-29.

Karama za Kiroho ni thibitisho la maisha yaliyojazwa Roho. Soma Matendo 2:4 na 1 Wakorintho 12:30-31. Inaweza kuwa mojawapo ya karama hizi, kama kuonena kwa lugha. Baadhi ya Wakristo wana karama hii hali wengine hawana. Mmoja anaweza kuwa na karama ya kuhubiri hali mwengine ya kufundisha.

Je! ni lini mtu hujazwa na Roho? Mtu hujazwa na Roho anapompokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wake, lakini huendelea kujazwa. Bwana huwapa Roho wale wanaofanya



Ni muhimu kujua kwamba majaribu si dhambi. Shetani atatujaribu jinsi alivyomjaribu Yesu Kristo, Bwana wetu. Hutujaribu tujivunie mambo ya kiroho au vyeo vyetu. (1 Timotheo 3:6)

Hutujaribu tutegemee hekima yetu, nguvu na utajiri. (2 Wakorintho 12:1-8; Mathayo 16:21-23)

Shetani hutumia kuanguka kwetu kutukatisha tamaa. Biblia inatwambia, "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote" (1 Yohana 1:9). Shetani huondoa upendo kati ya Wakristo na kuleta migawanyiko. Hujaribu kuleta migawanyiko kati ya viongozi wa kanisa na kuwafanya Wakristo wachukiane.

Tumeona kwamba Shetani humpinga Mungu. Kwa sasa anajenga ufalme wa kumpinga Mungu ndani ya mioyo ya watu wasio watiifu. (Waefeso 2:1-3) Kazi yake yote ni ya kumpinga Mungu. Tunajua kwamba Mungu ni pendo na anataka watu wapendane. Lakini Shetani anataka kuwaona watu wakichukiana.

Shetani hupinga yote Mungu anayofanya. Huwafanya watu wamwasi Mungu badala ya kumtii. Wengi hukataa kumpokea Yesu kuwa Mwokozi wao kwa sababu wamefungwa na Shetani. Huwafanya watu wengi kufuata mafundisho maovu. Kwa mfano, watu wengi wanaamini kwamba wanaweza kupata haki ya Mungu kwa kutenda mema (1 Timotheo 4:1-3; Waefeso 2:8-9), au kwa kutii Sheria. (Warumi 3:20)

Watu wengi wamekuwa vipofu kiasi kwamba hawawezi kukubali "...haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo..." (Warumi 3:22) na kukubali wokovu katika Yesu Kristo. (Matendo 4:12) Mungu anataka kila mmoja aokoke (1 Timotheo 2:4), lakini Shetani huwadanganya wengi wakatae

kuokoka. Kwa kuwa umejua yale anayofanya Shetani, unaweza sasa kujihadhari naye.

**KAZI YA KUFANYA**

1. Andika orodha ya vifungu vyote vya Biblia vinavyozungumzia juu ya Shetani.

2. Mwombe Mungu akuonyeshe njia ambazo Shetani anajaribu kukudanganya.

3. Mwombe Mungu akupe nguvu za kumpinga Shetani.

4. Mwambie mtu mwingine yale umejifunza kuhusu Shetani.

## SURA YA TATU

# SHETANI NA HUKUMU

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitaelewa kwa nini Shetani anatujaribu na jinsi atakavyoshindwa na Mungu wakati wa hukumu.

SOMO KUTOKA: Ufunuo 19:11-21, 20:1-9; Ayubu 1:6-12; Mathayo 25:41

VIFUNGU VYA LEO: Ufunuo 20:1-9

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "...Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi" (1 Yohana 3:8).

**KUSOMA SOMO**

**UTANGULIZI**

Siku ilifika ya kusikiliza kesi ya kijana jahili ambaye alimpiga mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule yao. Alipoulizwa sababu ya kuwapiga wengine, alijibu kwamba ni



Ufisadi inamaanisha kulewa kabisa au kutenda maovu.

Paulo alikuwa akitoa muhtasari wa yale aliyosema. Alikuwa akisema kwamba tusijazwe na hasira, wizi, uongo, uchungu, ghadhabu, uzinzi na matukano. Tunapaswa kuacha mambo haya. (Waefeso 4:25-32) Paulo aliendelea kusema, "...mfanywe wapya katika roho..." (Waefeso 4:23). Alikuwa anasema katika kifungu cha 2 kwamba Wakristo wanapaswa kuchukuliana katika upendo. Upendo ndio dhihirisho la maisha yaliyojaa Roho. Hii ni kusema kwamba Mkristo aliyejazwa Roho ndiye awezaye kuenenda kwa upendo. Mtu akiwa hajajazwa Roho huenenda kwa mwili na maovu.

Kujazwa na Roho inamaanisha kuongozwa na kutawaliwa na Roho Mtakatifu. Humtawala Mkristo ili asiishi maisha ya kimwili. Humwongoza Mkristo kuishi maisha ya upendo. Je! mtu anawezaje kujazwa na Roho? Yohana 7:37-39 inasema, "...Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na neno hili alilisema katika habari ya Roho...." Yesu alifundisha mambo haya wakati wa sikukuu ya vibanda. (kifungu cha 2) Wayahudi walimwaga maji chini kila asubuhi kabla ya kuanza shughuli zo zote. Hili lilikuwa sala kwamba Mungu atatuma mvua ya kutosha. Wayahudi waliamini kwamba mavuno yalitegemea wingi wa mvua.

Huu ni mfano mzuri wa maisha ya Kiroho. Unamaanisha kwamba anataka kuenenda na Mungu. Pili, mtu anapaswa kutubu na kumwendea Yesu. Anapaswa kukiri dhambi zake na kuziacha. Tatu ni lazima amfanye Kristo awe Bwana wake. Nne, ni lazima umwamini Kristo kutawala na kuongoza maisha yako. Imani na utii hutuwezesha kujazwa na Roho. Si kwa kuhisi au kwa matendo au kutii sheria.

Je! ni nini dhihirisho la maisha yaliyojaa Roho? Tunda la Roho huonyesha maisha yaliyojaa Roho. Soma Wagalatia

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa" (Mathayo 7:7).

## KUSOMA SOMO

### UTANGULIZI

Yohana alifurahi sana. Alikuwa amefanya kazi kwa miaka mingi na kuweka akiba ya pesa za kutosha kununua gari lake la kwanza. Halikuwa gari jipya lakini lilimpendeza sana Yohana.

Hakuwa amefika mbali wakati lilipogoma kwenda. Hakujua kilichofanyika, lakini akaendelea tu kuliendesha. Mwishowe lilisimama tena na kushindwa kwenda. Je! ni nini kilichofanyika kwa gari la Yohana? Alilisukuma na kuliondoa barabarani. Kisha akaanza kuwaza.

Rafiki yake Yakobo, alifika wakati huo aliposimama kando ya gari lake. "Je! kuna nini?" Yakobo akamwuliza.

Yohana alimwelezea kila kitu, halafu Yakobo akaingia garini. Yakobo aliwasha moto gari hilo na kumwmbia Yohana kwamba halina mafuta. Gari halikuwa limeharibika ila halikuwa na nguvu za kwenda. Halikuwa na mafuta.

Gari hilo lilianza kwenda Yohana alipolitia mafuta.

Wakristo wanahitaji nguvu maishani mwao. Nguvu hii ni Roho Mtakatifu aishiye ndani yao. Mkristo hawezi kufanya kazi bila nguvu hii. Anahitaji kujazwa na Roho Mtakatifu. Hebu tujifunze habari yake.

### MAELEZO

Je! inamaanisha nini kujazwa na Roho Mtakatifu? Waefeso 5:18 inasema, "Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho."



kwa sababu hatapita mtihani wake wa mwisho wa mwaka. Kwa hivyo kusudi lake lilikuwa kuwapata marafiki ambao wataanguka pia. Kamati hiyo waliposikia jibu lake, walimsikitikia sana kijana huyo.

Hii inatukumbusha kwamba Shetani amejaribu kupanga njia za kumdanganya mwanadamu kwa sababu anajua kwamba atashinda. Tunaweza kuona tunaposoma vifungu vya Ufunuo kwamba kutakuwa na kilio kikuu siku ya hukumu.

Mungu ametupa nafasi ya kutayarisha jeshi lake ambalo litapigana vita vya mwisho. Shetani atashindwa kabisa.

Mungu hatuachi peke yetu. Hutusaidia kushinda majaribu ya Shetani.

### MAELEZO

Je! Shetani ni nani? Mwandishi wa Ayubu anatuambia kwamba yeye ni mkuu wa roho walioanguka, adui wa Mungu na mwanadamu. Tunasoma katika Ufunuo 12:10 kwamba Shetani ni mshitaki wa ndugu zetu. Soma sura ya kwanza ya kitabu hiki tena kukukumbusha jua ya Shetani.

Mungu alimfukuza Shetani kutoka mbinguni kwa sababu ya maasi yake. Shetani aliamini (na bado anaamini) kwamba anaweza kumpindua (kumshinda) Mungu ili awe na mamlaka, lakini wakati huo hakuwa na mamlaka juu ya uwezo wake. Alihitaji wakati wa kuwa duniani. Mungu amemwacha Shetani atayarishe jeshi lake la kupigana vita vya mwisho, wakati ambapo Shetani ataangamizwa kabisa. Anatumia hila na ujanja kwa kumdanganya mwanadamu.

Soma Ufunuo 19:11-21. Mfalme aliye mwaminifu na wa kweli huhukumu na kufanya vita. Jeshi la mbinguni watatawala kwa uwezo mkuu chini ya uongozi wa Bwana wa mabwana.

(kifungu cha 14) Wasiowaamini watakuwa na wakati mgumu wakati Bwana atatayarisha jeshi lake kupigana vita.

Kulingana na vifungu vya 19 na 20, Shetani na jeshi lake watashikwa na kutupwa kwenye ziwa la moto liwakalo kwa kiberiti.

Kifungu cha 21 kinasema, waliochini ya utawala wa Shetani wauawa kwa upanga wa Bwana.

Kazi ya Shetani itaangamizwa. Hii ndiyo sababu Yesu alikuja kutimisa ahadi yake. Ataarudi tena duniani. Mtu asipomwamini Yesu, kutoamini kwake kunamweka upande wa Shetani. (Yohana 3:18)

Shetani hafurahii tunapomwamini Yesu. Huanza kutujaribu tufanye dhambi. Yohana 16:11 inatuonyesha kuwa Shetani amekwisha kushindwa na kuhukumiwa.

Ayubu alikuwa mtumishi mwaminifu wa Mungu, lakini alijaribiwa. Kila mtu hujaribiwa. Lakini Mungu atampa mtu uwezo wa kumshinda Shetani kama amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi.

Jehanum ni mahali palipotengenezewa ibilisi. Mungu hataki mtu ye yote kwenda huko. Yeye "...hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli" (1 Timotheo 2:4). Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee kumtengenezea mwanadamu njia ya kuwa na uzima wa milele. Soma Yohana 3:16. Ni lazima kila mmoja achague yule atakayemfuata.

Ni lazima uchague yule utakayemfuata kwa sababu hutachaguliwa na mtu ye yote.



Atakuhimiza katika mawazo na moyoni. Atakupa ujasiri wa kushuhudia. Atakushauri wakati wa shida. Atakusaidia kuomba na kuelewa Neno la Mungu. Ni muhimu kumwomba Roho Mtakatifu akuongoze unaposoma Biblia yako. Roho huwasaidia waamini kumpenda Mungu, watu wengine na wewe mwenyewe. Kwa hivyo wewe kama Mkristo unapaswa kusema, "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu" (Wafilipi 4:13).

**KAZI YA KUFANYA**

1. Ikiwa umempokea Yesu Kristo, amini kwamba Mungu alikupa Roho Mtakatifu wakati huo. Sasa anaishi ndani yako. Akakubadilisha uwe kama Kristo na kuyafanya mambo yote katika Kristo. Jitoe na umtii Roho wakati wote. Ndipo atakubadili uwe kama Yesu Kristo.

2. Mtegemee Roho unapoomba na kusoma Biblia yako. Mwombe akusaidie kuelewa Neno lake. Usimuudhi Roho Mtakatifu.

3. Mwamini Roho Mtakatifu unapowashuhudia wengine kwa sababu ndiye huwavuta wenye dhambi kwa Kristo.

## SURA YA KUMI NA MOJA

# KUJAZWA NA ROHO MTAKATIFU

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza maana ya kujazwa na Roho Mtakatifu.

SOMO KUTOKA: Yohana 7:37-39; Wagalatia 5:22-23

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 7:37-39; Wagalatia 5:22-23

## MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Watu ambao hawajampokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wao hawana Roho Mtakatifu. Anawapenda na hujaribu kuwaonyesha kwamba wamepotea, lakini hawajampokea maishani mwao. Wanaishi maisha ya gizani. Kwa hivyo wanapaswa kupokea Yesu maishani mwao. Watabadilika wakikata shauri hilo. Nao watampokea Roho Mtakatifu. Je! utakata shauri leo kama hujampokea Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wako?

Kuzaliwa mara ya pili hutokea mtu anapompokea Kristo. Huzaliwa upya katika Roho. (Yohana 3:3-5) Kazi ya kwanza ya Roho katika maisha ya mtu ni kumshawishi ampokee Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wake.

Roho huhusika katika kubadilisha maisha yetu. Humfanya mtu kuwa kiumbe kipya. Biblia inatwambia kuhusu kiumbe kipya. Tunasoma katika 2 Wakorintho 5:17, "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! yamekuwa mapya." Uumbaji mpya uko katika Yesu Kristo. Huanza wakati wa kuzaliwa mara ya pili. Ni kupitia kwa Neno la Mungu (Yesu Kristo) na uwezo wa Mungu (Roho Mtakatifu). Roho hutumia Neno la Mungu alilosikia mwamini na kumbadilisha. Hii inamaanisha kwamba utabadilishwa unaposema au unaposikia Neno la Mungu. Utabadilishwa na kuwa kama Yesu. (Warumi 8:29)

Je! ni nani anayekubadilisha? Roho Mtakatifu aliyeanza kazi njema maishani mwako ataitimiza. (Wafilipi 1:6) Je! ataitimiza lini? Biblia inasema kwamba ataitimiza siku ya Yesu Krsito. Je! kwa nini ataitimiza? Ili uweze kufikia mahali alipokutayarishia mbinguni. (Yohana 14:2-3)

Roho ni msaidizi na mshauri wetu. Roho Mtakatifu atakuongoza yale ya kufanya kama anaishi ndani yako.



## MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Je! unaelewa maana ya Shetani na hukumu? Shetani alifukuzwa kutoka mbinguni kwa sababu ya kuasi kwake. Alitaka kupindua utawala wa Mungu ili atawale.

Unapaswa kujua kwamba Mungu hamwogopi Shetani. Biblia inatufundisha kwamba Shetani ameshindwa. Amekwisha hukumiwa. Yohana 16:11 inasema, "...amekwisha kuhukumiwa."

Kila mmoja wetu ana hatia ya dhambi. (Warumi 3:23) Lakini Mungu anataka tusamehewe ili tusione haya wakati wa hukumu.

7Mungu anakupenda kiasi kwamba alimtoa Mwanawe pekee akuokoe mautini. Alikufa msalabani ili upate uzima wa milele. Atakupa nguvu za kushinda majaribu ya Shetani.

Mungu alimruhusu Ayubu aharibiwe, (Ayubu 1:12) atikiswe, lakini Ayubu alikuwa imara na mwaminifu. Shetani anapokutikisa maishani ni lazima ukumbuke kwamba unayo nguvu katika Yesu na unaweza kubakia imara.

Mungu anaweza kusamehe dhambi yo yote mtu anapotubu na kumpokea Kristo kuwa Bwana na Mwokozi. Unapomwamini utatambua kwamba hakosi kumtimiza ahadi zake kwako.

Jehanum haikutayarishiwa mwanadamu. Ilitayarishiwa ibilisi. Mwanadamu ataenda Jehanum kwa sababu anatii Shetani badala ya kumwamini na kutii Yesu Kristo.

Huu ndio wakati wa kuepuka hukumu ya Mungu. Mungu atakusaidia kama utamtegemea. Mkubali leo mwanawe, Yesu, kuwa Mwokozi wako.

**KAZI YA KUFANYA**

1. Mwombe Mungu akusaidie kuelewa vifungu vya somo hili na maana yake.
2. Mwombe akusaidie kuwa na hakika kwamba uko tayari kwa hukumu.
3. Mwombe Mungu akutumie kumsaidia mtu mwingine kujitayarishia hukumu.

## SURA YA NNE

# UCHAWI NA KAZI YA SHETANI

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza jinsi Shetani anavyotumia uchawi kufanya kazi yake.

SOMO KUTOKA: 2 Mambo ya Nyakati 33:1-6; Kutoka 22:18; Matendo 16:16-18; 2 Wakorintho 11:13-15

VIFUNGU VYA LEO: 2 Mambo ya Nyakati 33:1-6; Kutoka 22:18; Matendo 16:16-18; 2 Wakorintho 11:13-15

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:"...Lakini Paulo akasikitika, akageuka akamwambia yule pepo, Nakuamuru kwa jina la Yesu Kristo, mtoke huyu. Akamtoka saa ile ile" (Matendo 16:18).

**KUSOMA SOMO**

**UTANGULIZI**

Rachel, mwenye miaka ishirini na mitano amezaa watoto wanne. Watatu kati yao walikufa kabla ya kutimiza mwaka mmoja. Amebaki mtoto mmoja ambaye huwa mgonjwa mara kwa mara. Rachel ameshauriwa na watu wengi wa kijiji aende kwa mchawi. Wamemhakikishia kwamba atatatua shida zake.



Kwa hivyo, Roho Mtakatifu alihusika katika kuzaliwa kwa Yesu.

Roho Mtakatifu alimtukuza Yesu katika huduma na maishani mwake. (Mathayo 3:13-17; Yohana 14:18-19) Alimwinua juu Yesu. Watu waliponywa na kupata uzima wa milele walipomjia Yesu. Yesu Kristo huponya na kutoa uzima wa milele kupitia kwa Roho Mtakatifu. Miujiza ya Yesu ilifanywa kwa uwezo wa Mungu. Ni muhimu kuona jinsi utatu (Baba, Mwana na Roho) ulivyoshirikiana pamoja. Roho Mtakatifu hufanya mapenzi ya Baba kupitia kwa Roho Mtakatifu.

Je! Roho Mtakatifu hufanya kazi gani katika maisha ya mwamini? Kwanza mtu huyo hangeamini bila ya Roho Mtakatifu. Roho Mtakatiku ndiye humwonyesha mtu kwamba ni mwenye dhambi na anahitaji Mwokozi. Roho humsaidia mtu kuelewa kwamba Mungu amewaletea waamini wote njia ya wokovu. Mungu hutumia Roho Mtakatifu kumfanya mwenye dhambi aamini kwamba Yesu alifia dhambi zake.

Roho Mtakatifu huishi ndani ya mwamini. Ni mshauri ambaye yuko wakati wote. Soma Yohana 14:16-20 na Warumi 8:6-14. Wakristo humpokea wanapomkubali Yesu kuwa Mwokozi wao. Roho Mtakatifu hajilazimishi kuingia ndani ya mtu. Kupokea Roho Mtakatifu ni sehemu moja ya kuongoka. Biblia inasema kwamba mtu asiye na Roho si wa Mungu. (Warumi 8:9b) Mtu hawezi kuwa Mkristo bila Roho.

Maneno ya Yesu katika Yohana yana maana kwamba Roho Mtakatifu ni msaidizi katika maisha ya mwamini. Waamini hushiriki ushindi wa Kristo kupitia uwezo wa Mungu, Roho Mtakatifu. Soma Warumi 8:10-11. Paulo anasema kwamba Baba ametupatia yaliyo ya Yesu. Kifo chake, kufufuka na haki yake huwa mali yetu. Baba hufanya hivyo kupitia kwa uwezo na Neno lake.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu" (Wafilipi 1:6).

**KUSOMA SOMO**

**UTANGULIZI**

Je! tunaweza kulinganisha nini na kazi ya Roho Mtakatifu? Hakuna kamwe! Hatuwezi kulinganisha kazi ya mwanadamu na kazi ya Roho Mtakatifu. Kazi ya mwanadamu haikamiliki. Je! unaona unapotazama mazingara yako? Mijengo ambayo haijakamilika, mashamba ambayo hayajalimwa, na kazi ambazo hazijaisha zinatukumbusha nia nzuri tulizonazo. Tunapanga kufanya mambo, lakini tunashindwa kukamilisha.

Kazi ya mwanadamu inaweza kuzeeka, kuchakaa na kuharibika. Inaweza kuharibiwa na moto, hali ya anga na kutumiwa vibaya. Lakini Roho Mtakatifu hukamilisha kazi yake. Haiachi nusu nusu. Kazi yake hudumu milele. Haiwezi kuzeeka wala kuharibiwa na moto au maji. Je! tunaweza kumpa Roho Mtakatifu kazi ipi? Hebu tujifunze kazi ya Roho Mtakatifu na jinsi inavyohusu maisha yetu.

**MAELEZO**

Mungu alipoumba ulimwengu, alisema tu kwamba, "...Iwe nuru..." (Mwanzo 1:3). Huu ni mfano mzuri wa kazi ya Roho Mtakatifu. Roho alitumia Neno la Mungu kuleta mabadiliko. Alitumia neno kuumba. Mungu aliposema, "Iwe nuru," uwezo wake (Roho) ulifanya maajabu ya kuleta nuru.

Utatu, yaani Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu, walishiriki katika kuzaliwa kwa Yesu Kristo. (Luka 1:35) Baba alipangia Mwanawe kufanyika mtu. Roho Mtakatifu alitimiza mpango huo na Mwana akafanyika mtu.



Hata wamemwambia mifano ya watu ambao wanadai wametatuliwa shida zao na wachawi.

Rachel ataitikiaje shida hii?

Watu tofauti wa makabila ya Kiafrika wanashiriki katika uchawi. Wanafikiri ndilo jibu la hofu, shida na matumaini yao.

Wachawi huamini nguvu za roho ambazo zaweza kutumiwa kupitia kwa wataalamu, vifaa au mila kwa kujistarehesha, kwa ulinzi na kutajirika. Uchawi huchukuliwa kama njia ya kuwadhulumu wengine. Wachawi hutumia hirizi na kudanganya. Tunaweza kujifunza kutoka kwa uchawi kazi za Shetani.

**MAELEZO**

Soma 2 Mambo ya Nyakati 33:1-6. Tunaona katika maandiko haya kwamba wachawi huamini na kuheshimu vitu badala ya Mungu. Manase aliamini Baali badala ya Mungu wa Israeli. Manase alianza kufanya uganga, kubashiri na uchawi.

Watu waliaamini na kuabudu Shetani. Hii ndiyo sababu Biblia inakataza uchawi.

Soma Kutoka 22:18. Mungu anachukia uchawi. Kulingana na Agano la Kale, wale waliofanya uchawi walihukumiwa kifo. Soma pia Mika 5:12 na Wagalatia 5:19-20.

Fungua sasa katika Matendo 16:16-18. Yule msichana kijakazi alifanya uaguzi chini ya uongozi wa pepo. Paulo alimtoa yule pepo kwa jina la Yesu Kristo. Maneno haya, "kwa jina la Yesu Kristo" yanaonyesha nguvu na tabia ya Yesu.

Kuna nguvu katika Yesu za kuwakomboa watu kutoka kwa mamlaka ya Shetani. Yesu anataka watu wasitawaliwe na pepo au roho wachafu. Paulo alikuwa na uwezo juu ya pepo kwa sababu alikuwa na Roho Mtakatifu. Waamini

wanakumbushwa katika 1 Yohana 4:4 kwamba Yesu aishiye ndani yao ni mkuu kuliko Shetani aliyeko ulimwenguni.

Soma 2 Wakorintho 11:13-15. Fungu hili linafundisha kwamba Shetani hujigeuza na kuwa mfano wa malaika wa nuru. Shetani ana uwezo. Hii ndiyo sababu anaweza kutumia vitu vya kuvutia kuwavuta watu kwake. Hutumia kila njia kutimiza kusudi lake.

Tunajifunza katika Yohana 10:10 kwamba kusudi kuu la Shetani ni kuangamiza maisha ya watu. Yote afanyayo Shetani yamejaa maovu. Shetani hutumia uchawi kama njia mojawapo ya kuangamiza maisha ya watu. Anaweza kudanganya na kutua ahadi za uongo. Alimdanyanyа Hawa katika bustani ya Eden kwa kumwambia atapata ufahamu kutofautisha mema na mabaya. Hawa alikosa baraka za Mungu kwa sababu alimtii Shetani.

Tendo moja la uchawi limewafanya watu wengi wategemee uchawi. Shetani anawatawala watu hawa.

**MAFUNZO YA SURA HII KWANGU**

Unahitaji kumwamini yule anayekutakia mema maishani. Shetani huja kuiba, kuua, na kuharibu, lakini Yesu alikuja ili uwe na uzima wa milele. Soma tena Yohana 10:10.

Shetani yungali anafanya kazi hata sasa. Kusudi lake kuu ni kutuangamiza. Hutumia nguvu na pepo wachafu kutushawishi tumwamini. Hutumia kila njia kutimiza lengo lake.

Shetani hutufunga tunapomruhusu atawale maisha. Hututenganisha na Mungu kwa kutudanganya.

Tunapoingilia uchawi, huanza kumwamini na kumheshimu Shetani badala ya Mungu. Mwishowe humuabudu Shetani. Lakini Biblia inakataza aina yo yote ya uchawi. Wanaofanya



kuwasaidia na kuwaondolea hofu yao. Atawabadilisha na kuwafanya wawe na ujasiri wa kushuhudia.

Je! una shida hii ya kuwa na hofu? Roho Mtakatifu atakusaidia. Je! utamwamini?

Roho Mtakatifu huwasaidia pia wasio waamini. Huwaonyesha dhambi zao na hitaji la Mwokozi. Huwasaidia kuelewa habari njema ya ufalme na kumwamini Mungu. Unaweza kuwaombea rafiki zako wasio Wakristo na kumwomba Roho Mtakatifu awaonyeshe dhambi zao na hitaji lao la wokovu.

**KAZI YA KUFANYA**

1. Panga wakati wa kuomba na kusoma Biblia kila siku. Mtegemee Roho Mtakatifu unapofanya hivyo. Atakusaidia kuomba jinsi unavyotakiwa. Atakusaidia kuelewa Biblia.

2. Anza kushuhudia pale ulipo. Inaweza kuwa nyumbani, shuleni, njiani au mahali po pote ulipo. Kumbuka kushuhudia kwa yale unayosema, unafikiria na unayofanya. Unaye msaidizi, Roho Mtakatifu.

3. Zungumzana na marafiki wasio Wakristo na uwashawishi kumpokea Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wao.

**SURA YA KUMI**

# KAZI YA ROHO MTAKATIFU

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza juu ya kazi ya Roho Mtakatifu maishani mwangu.

SOMO KUTOKA: Luka 1:35, Mathayo 3:13-17; Yohana 14:16-20; Warumi 8:6-14

VIFUNGU VYA LEO: Luka 1:35, Mathayo 3:13-17, Yohana 14:16-20; Warumi 8:6-14

ulimwengu. Lakini mambo yanayoleta thamani maishani ni kumpenda Mungu na mwanadamu. Roho huwasaidia watu kuelewa kwamba tutasimama mbele ya kiti cha Mungu naye atatuhukumu. Roho Mtakatifu angewaongoza wanafunzi katika ukweli wote. Soma kifungu cha 13. Wangejifunza maana ya kuteswa kwa Kristo, kifo na kufufuka kwake.

Tunaona katika Agano la Kale kwamba Roho alifanya kazi kupitia kwa manabii, makuhani, wafalme na viongozi maalum. Lakini sasa watu wote po pote walipo wanaweza kupokea Roho Mtakatifu. Yeye alikuwepo kufanya kazi maalum lakini hakukaa nao milele. Roho wa Mungu ametolewa kama kipawa kwa wale wanaompokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi. Hukaa milele katika waamini wote na kufanya kazi kupitia kwao.

**MAFUNZO YA SURA HII KWANGU**

Roho Mtakatifu ni uwezo wa Mungu unaotolewa kwa Wakristo wote. Mungu huwapa kipawa wote wanaompokea Yesu kuwa Mwokozi wao. Kipawa kile ni Roho Mtakatifu anayekaa ndani yako wewe kama Mkristo. Mwili wako ni hekalu la Roho Mtakatifu.

Mungu Baba na Mungu Mwana wako ndani yako kupitia kwa Roho. Hii inamaanisha kwamba Mungu anaishi ndani yako. Hupenda kushiriki nawe. Anakutarajia umwombe. Anakutarajia umsikilize anaposema nawe. Mungu hunena na watu wake kupitia kwa Neno lake na watu wengine. Hutumia pia njia zingine kama shida na mahitaji.

Roho Mtakatifu yupo kukusaidia katika kazi aliyokupa. Anataka akusaidie kumshuhudia Kristo na kuhubiri habari njema ya ufalme wa Mungu.

Watu wengi huogopa sana kushuhudia na kuhubiri. Wakristo kama hao hawajatambua kwamba Roho Mtakatifu yuko tayari



uchawi tayari wamehukumiwa kifo. Shetani anaweza kututumia kama hatutajihadhari.

Tunapaswa kukumbuka kwamba Yesu ana nguvu za kututoa katika vishawishi vya Shetani. Ana uwezo mkuu kuliko Shetani aliyeko duniani. Wakristo wana ushindi kwa sababu Yesu ameushinda ulimwengu. Ametuondoa katika mambo ya uchawi, ulozi na kubashiri. Roho Mtakatifu atatuongoza katika ukweli tunaporuhusu atawale maisha yetu.

Je! maisha yako yanatawaliwa na Roho Mtakatifu au Shetani? Mshinde Shetani kwa kuyatoa maisha yako leo kwa Yesu Kristo. Anabisha mlangoni pa moyo wako. Ataingia ndani kama utamfungulia. Chukua leo hatua hiyo ya imani.

**KAZI YA KUFANYA**

1. Fikiria leo juu ya hofu na shida zako. Je! unatarajia kufanya nini siku zijazo? Chukua kalamu na karatasi na uandike mambo hayo.

2. Omba na umwambie Yesu mambo haya na uamii kwamba atakutimizia. Tafuta rafiki yako Mkristo au mwalimu wako wa Biblia na mwombee pamoja mambo haya.

## SURA YA TANO

# JINSI YA KUTAMBUA UCHAWI

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza jinsi nitakavyo tofautisha na kutambua uchawi.

SOMO KUTOKA: Yeremia 27:5-9; Danieli 2:27-28; Isaiah 2:5-6; 1 Yohana 4:1-6

VIFUNGU VYA LEO: Yeremia 27:5-9; Danieli 2:27-28; Isaiah 2:5-6; 1 Yohana 4:1-6

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:** "Basi matendo ya mwili ni dhahiri,...uchafu,... uchawi,...watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu" (Wagalatia 5:19-21).

**KUSOMA SOMO**

**UTANGULIZI**

Simoni anaugua ugonjwa wa UKIMWI. Amewaendea madaktari wote mjini. Lakini hajapata nafuu. Mama yake Simoni alimwambia kwamba atampeleka mahali ambapo atatibiwa. Walifunga safari na kwenda kijiji. Walipofika walikaribishwa katika nyumba ya nyasi kwa karuka vifaa tofauti vya kienyeji. Simoni alianza kushangaa yule ni daktari wa aina gani. Kisha akatambua kwamba wamemwendea mganga.

Je! utafanyaje ukiwa katika hali ya Simoni? Je! unawezaje kutofautisha mganga na daktari wa kienyeji?

**MAELEZO**

Uchawi na uganga unafanywa katika sehemu nyingi za Afrika. Wachawi hudai kwamba wanaweza kutatua shida za maisha. Wao hudai kwamba wanaweza kuponya na kuloga. Mambo haya mawili huwa yanapingan'a.

Wachawi husema kwamba wana nguvu za aina fulani. Hutumia vifaa vya kiajabu kubashiri yatakayofanyika, kuona ulozi, kutambua ugonjwa na kuharibu mazingara kwa kujifaidi.

Biblia inatumia maneno haya, uchawi, ulozi, ubashiri na uaguzi kama mawakilishi wa uchawi. Haya ni majina yanayotumiwa kumaanisha uchawi. Wachawi hutumia madhabahu, hirizi, tambika, zingiro, sihiri na vifaa vingine.



Wataletewa kama wako tayari kulipa gharama yake. Hapo ndipo itawafanyia kazi.

Roho Mtakatifu ni uwezo wa Mungu. Yeye ni kama nguvu ya umeme. Yeye yupo, lakini ni lazima mtu aamue kama atamtumia.

Je! Roho Mtakatifu alikujaje ulimwenguni? Je! ana kazi gani katika maisha ya Mkristo? Je! kwa nini Roho Mtakatifu alikuja? Hebu tujifunze habari zake.

**MAELEZO**

Yesu alizungumza na wanafunzi wake akiwaelezea kuhusu kifo chake. Aliahidi kwamba mshauri atakuja kwa sababu, "...nitampeleka kwenu" (Yohana 16:2). Hii ni ahadi ya ajabu! Ilimaanisha kwamba Baba na Mwana watakuwepo kwa wanafunzi katika Roho. Hivi ndivyo Baba alikuwepo wakati wa huduma ya Yesu. Wanafunzi wangesaidiwa kwa sababu Roho angekuwa pamoja nao na kufanya kazi kupitia kwao.

Roho Mtakatifu angewasaidia wanafunzi katika kazi yao. Kazi yao ilikuwa kumshuhudia Kristo na kuhubiri habari njema ya ufalme wa Mungu. Roho huwasaidia watu kuelewa habari njema na kuitikia Mungu kwa imani.

Vifungu vya 8-11 vinasema Roho Mtakatifu atauhakikishia ulimwengu habari ya dhambi, na haki na hukumu. Kuuhakikishia ulimwengu habari ya dhambi kuna maana ya kuwasaidia wapotevu kumpokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yao.

Kuuhakikishia ulimwengu habari za haki kunamaanisha kwamba Roho atawafanya watu waamini kumtii Kristo. Kuuhakikishia ulimwengu hukumu kunamaanisha kuwasaidia watu waelewe kwamba wote watahukumiwa na Mungu. Mambo yaletayo maovu maishani ni mali na anasa za

3. Jitoe kukariri kifungu kimoja kila wiki. Tafuta mtu wa kukariri naye na kusahihishiana.

4. Jaribu kufikiria kila wakati Neno la Mungu. Mwache akufundishe yale anayotaka ufahamu.

5. Mwambie mtu mmoja kila wiki yale ambayo Mungu anakufundisha kutoka kwa Neno lake.

### SURA YA TISA

## KUJA KWA ROHO MTAKATIFU

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza maana ya kuja kwa Roho Mtakatifu.

SOMO KUTOKA: Yohana 16:7-13; Matendo 2:14-21

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 16:7-13; Matendo 2:14-21

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Na itakuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa" (Matendo 2:21).

KUSOMA SOMO

UTANGULIZI

! Umewahi kufikiria juu ya nguvu za umeme zilizoko katika miji siku hizi? Umeme una matumizi mengi nyumbani. Hutoa mwangaza hutumiwa kwa kupika, kuosha, kufagia na kazi zingine nyingi.

Watu wengi hufurahia kuwa na umeme nyumbani kwao. Huwasaidia kufanya kazi. Lakini baadhi ya watu hawana umeme huu. Hawawezi kulaumu umeme kutokuwa nyumbani kwao. Lakini ni kwa sababu hawajawekewa nyumbani kwao. Uamuuzi wa kupewa umeme ni wa mwenye nyumba.



Ni vigumu siku hizi kutambua uchawi na wachawi. Uchawi umeendelea zaidi. Wachawi wanafanyia uchawi katika nyumba za kisasa badala ya nyumba za matope na nyasi.

Ni muhimu kutofautisha uchawi na madaktari wa kienyeji. Makabila mengi yana waganga wa kienyeji. Wengi kati ya waganga hawa si wachawi.

Je! mtu anawezaje kutofautisha waganga wa kienyeji na wachawi? Biblia inazungumzia kuhusu uchawi. Tunaweza kufanya uamuzi juu ya uchawi kwa kutumia neno la Mungu.

Soma Yeremia 27:5, 9-10. Wachawi hasa hudanganya watu. Huwaambia yale wanayotaka wasikie. Huahidi watu afya nzuri, utajiri na fanaka. Lakini wachawi hawana uwezo wa kufanya mambo haya yatendeke.

Soma Yeremia 29:11. Ahadi hii ya Mungu kwa Israeli ni ya kweli kwa wale wanomwamini Mungu. Afya nzuri na baraka ni zawadi kutoka kwa Mungu wala huwezi kuvipata kutoka kwa wachawi.

Fungua Danieli 2:27-28 na Isaya 2:5-6 na usome vifungu hivi. Maandiko yanatufundisha kwamba wanadamu hawawezi kutambua siri ya maisha. Mungu wa mbinguni anaweza kufanya yale ambayo wanadamu hawawezi.

Soma 1 Yohana 4:1-6. Maandiko haya yanatwambia jinsi ya kujaribu roho. Je! kujaribu ni nini? Kanuni zilizoko katika vifungu hivi ni za kutusaidia kutofautisha waganga wa kienyeji na wachawi.

Kwanza, kila roho inayokiri kuwa Yesu Kristo amekuja katika mwili ni ya Mungu. Wachawi husifu miungu na humkataa Kristo.

Kila roho ambayo hamkiri Yesu kuwa ni Mungu si ya Mungu. Wachawi hawamkiri Kristo kuwa Mungu. Wao huwapinga wanaomkiri Kristo.

Tatu, wale walio wa Mungu hukubali mafundisho ya mitume. Lakini wachawi hawaheshimu Neno la Mungu.

Je! kwa nini uchawi unafaulu mara kwa mara?

1. Ulinganifu: Kwa mfano watu wanaoamini uchawi, huamini kwamba wanyama fulani huleta mikasa mibaya. Wakati mwingine jambo baya hulingana na tendo baya. Wakati mwingine mambo haya mawili hufanyika wakati mmoja.

2. Mawazo: Mtu anapoambiwa amelogwa huwa na hofu nyingi mpaka huanza kuwa mgonjwa.

3. Nguvu za Kishetani: Shetani ambaye hujifanya kuwa "malaika wa nuru" anaweza kufanya mambo ya kuwavutia watu. Shetani anauwezo wa kufanya ishara na anaweza kuzitumia ishara hizi kuwanasa watu. Huzitumia kuangamiza maisha ya watu wanapovutiwa na ishara hizi.

**MAFUNZO YA SURA HII KWANGU**

Je! unawezaje kutambua waachawi, waaguzi na walozi? Njia moja ya kutambua watu hawa ni mavazi yao na vifaa wanavyotumia. Hutumia vifaa vya kuwavulia wale wanaowatembelea. Wao hudai kwamba wanaongozwa na roho. Huamini roho (pepo) na kuwasikiliza. Huwafanya watu waogope na kuamini pepo.

Biblia inatuambia kuhusu watu wachawi. Hudai mambo fulani, lakini hawawezi kuonyesha matokeo yake. Huwadangaya watu na kuwaambia yale wanayotaka wasikie. Huwaahidi watu kwamba watatajirika, wataishi maisha mazuri na watafanikiwa. Hudai kwamba wanatatua shida za maisha.



la Mungu? Ni lazima umtegemee ukitaka kuelewa Neno la Mungu.

Neno la Mungu linahusu maisha. Lina mafundisho ya kufuata maishani. Je! una Neno la Mungu maishani mwako? Unaweza kuweka Neno la Mungu maishani mwako. Hivyi ndivyo unavyopaswa kufanya:

1. Soma Biblia yako kila wakati. Jaribu kufahamu yaliyomo.

2. Jifunze Neno. Unaweza kutumia dakika kumi na tano kila siku kujifunza sehemu fulani ya Maandiko. Jifunze hasa kiini, maandiko na jinsi ya kuyatumia maishani mwako. Tunasoma katika 2 Timotheo 2:15, "Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli."

3. Kariri vifungu vya Biblia. Soma Zaburi 119:11. Haitoshi tu kusoma. Kujifunza na kukariri Maandiko. Je! unapaswa kufanya nini?

4. Ifikirie. Je! inahusuje maisha yako.

5. Mwishowe, tenda jinsi unavyojifunza. Kwa mfano, ukisoma amri ya Mungu juu ya kumpenda jirani yako, jaribu kufanya jambo la kuonyesha upendo.

Neno lenye pumzi ya Mungu hugusa maisha yetu. Huonyesha matendo ya Mungu yaliyoko ndani yetu wakati mtu anapoliruhusu kukua maishani mwake.

**KAZI YA KUFANYA**

1. Jitoe kusoma Neno la Mungu. Tenga wakati fulani kila siku wa kusoma Biblia.

2. Mwombe Mungu akusaidie kujifunza Neno lake. Panga wakati wa kusoma. Chagua kisa au kitabu unachotaka kusoma. Tafuta mwongozo wa kukusaidia kusoma.

Petro anasema kwamba walioandika hawakutumia maarifa yao wenyewe. Waliongozwa na Roho Mtakatifu na wakazungumza kwa niaba ya Mungu. Roho Mtakatifu ndiye aliyekuwa kiongozi wao. Aliwasaidia waandishi hao kuandika yale yaliyoko katika Biblia. Roho Mtakatifu ndiye hutusaidia kuelewa maana ya Maandiko.

Yesu aliahidi, "Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote;..."(Yohana 16:13).

Biblia, Neno lenye pumzi ya Mungu, limetoka kwa Mungu na ndiyo mamlaka ya maisha yetu. Tunajifunza katika Biblia kuhusu Mungu na maisha yetu. Paulo alisema Maandiko ni muhimu katika sehemu nne:

1. Kwa mafundisho: Yanawashauri waamini kuhusu Mungu.

2. Kuonya: Kuonyesha na kukataa makosa.

3. Kuongoza: Kusahihisha watu makosa yao na kuwaonyesha njia ya kufuata.

4. Kuandibisha katika haki: Kufundisha matendo na tabia nzuri.

Ni lazima Neno la Mungu liguse maisha yetu. Hapo ndipo mtu atakuwa kamili, wa kutenda kila tendo jema.

**MAFUNZO YA SURA HII KWANGU**

Biblia ni kitabu maalum ambacho ni tofauti na vitabu vingine. Ni Neno la Mungu. Ni mamlaka ya maisha yetu na tunastahili kutii mafundisho yake. Mafundisho ya Biblia yamezidi maoni ya mwanadamu.

Roho Mtakatifu ndiye mfafanuzi mwema wa Biblia. Huishi ndani ya wote waliomwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi. Huwaongoza katika ukweli wa Mungu. Je! huwa unamwomba Roho Mtakatifu akuongoze na akufundishe unaposoma Neno



Hudai pia kwamba wana uwezo wa kuponya. Lakini watu hawa hawawezi kutimiza mambo haya.

Mungu amesema katika Yeremia 29:11 kwamba yeye hutubariki kwa sababu anatujua. Anajua mahitaji na shida zetu. Hatuwezi kufanikiwa wala kuwa na matumaini mazuri kwa kuwaamini wachawi. Mungu hapendi wale wanaotumia nguvu za Shetani.

Kumbuka jaribio kuu la kutambua uchawi. Je! huwa wanamheshimu na kumtukuza Mungu? Je! huwa wanatii Neno lake? Maswali haya yatakusaidia kujua ukweli.

Mungu tu ndiye awezaye kufanya yale ambayo wanadamu hawawezi. Hutupa Roho anayetusaidia kutofautisha madakitari wa kienyeji na wachawi.

Mungu anawaita watoto wake, waenende "...katika nuru ya Bwana" (Isaya 2:5). Atatupa nuru yake kama tutamwomba kwa imani.

Soma Isaya 1:19-20. Maandiko haya yanatuonyesha kwamba ni lazima tukate shauri. Mungu anataka tumwendee ndipo atusamehe dhambi zetu, lakini hatulazimishi kamwe. Anatuita tuwaache roho wachafu ambao watatusumbua na tumfuate Roho Mtakatifu atakayetuongoza. Je! utachagua lipi?

**KAZI YA KUFANYA**

1. Je! umewahi kushiriki katika uchawi wo wote? Mwombe Mungu akusamehe dhambi hiyo.

2. Andika majina ya rafiki zako ambao utawaambia uwezo na matumaini katika Yesu, ili wasiuendee uchawi. Fikiria jinsi utakavyozungumzana nao kuhusu maisha yao.

3. Andika vifungu vya Biblia ambavyo vitakusaidia kujibu maswali yao yanayohusu jambo hili.

## SURA YA SITA

# UCHAWI NA MKRISTO

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitaelewa kwamba Ukristo hauuhisiani kamwe na uchawi.

SOMO KUTOKA: Kumbukumbu la Torati 18:10-12; Amosi 3:3; Mika 5:12; Marko 5:1-13; Matendo 8:9-24; 13:6-11;16:16-18; Waefeso 6:10-17

VIFUNGU VYA LEO: Kumbukumbu la Torati 18:10-12; Marko 5:1-13, Matendo 8:9-24; 13:6-11; 16:16-18, Waefeso 6:10-17

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:"Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani" (Waefeso 6:11).

**KUSOMA SOMO**

**UTANGULIZI**

Mzee kikongwe alilala kitandani kwa siku mbili. Alioonekana kwamba hataamuka tena. Kisha siku moja akatembelewa na mchawi. Kijana mdogo alimwona huyo na akaogopa sana. Alishangazwa na mavazi ya ajabu aliyovaa na vifaa vilivyoning'inia mwilini alipotembea. "Je! kwa nini mchawi anavaa mavazi kama haya na kujichora usoni?" kijana akajiuliza.

Mama yake alishindwa jinsi ya kumjibu. Akamwambia, "Wao huvaa hivyo ili watu wawaogope. Hufikiri kwamba watu watawaamini wakiwaendea hivyo."

Mungu aliwachagua wana wa Israeli kuwa watu wake maalum. Jambo moja ambalo Mungu alitarajia kutoka kwa watoto wake



utakutana na watu kama hao. Hebu sasa tuiangalie Biblia hiyo. Tutaona kwamba sio tu mawazo na mashauri ya watu. Hatimaye utaweza kuwajibu watu kama hawa.

**MAELEZO**

Biblia ni Neno la Mungu. Roho Mtakatifu ndiye aliyewawezesha wanadamu kuandika Neno la Mungu, na hutusaidia kuelewa Biblia. Yaliyoandikwa katika Biblia yanahusu maisha yetu. Biblia ina vitabu 66. Vitabu hivi vyote viliandikwa wakati tofauti. Viliandikwa na wanadamu walioongozwa na Roho Mtakatifu katika kipindi cha muda wa miaka elfu moja na mia tano. Hataingawa waliandika wakati tofauti, Biblia ni kitabu kimoja. Inazungumzia jambo moja na ukweli ule ule.

Je! inawezekanaje kuwa hivyo? Roho Mtakatifu ndiye aliyeongoza uandishi wake. Paulo anasema katika 2 Timotheo 3:16-17, "Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."

Tunajifunza katika 2 Petro 1:20-21, "...hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu."

Vifungu hivi viwili vinasisitiza kwamba Maandiko ni zaidi ya mawazo ya wanadamu, hata ingawa Mungu aliwatumia kuandika. Paulo alitumia maneno, "lenye pumzi ya Mungu." Hii ni tafsiri ya neno la Kiyunani. Inamaanisha kwamba Mungu alitayarisha wakati, watu na ujumbe wa Biblia.

SURA YA NANE

## ROHO MTAKATIFU NA UONGOZI

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitaelewa mamlaka ya Maandiko na umuhimu wake maishani mwangu.

SOMO KUTOKA: 2 Timotheo 3:14-17; 2 Petro 1:19-21

VIFUNGU VYA LEO: 2 Timotheo 3:14-17; 2 Petro 1:19-21

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu" (2 Petro 1:21).

KUSOMA SOMO

UTANGULIZI

Yakobo alikuwa akizungumza na baba yake siku moja jioni. Yakobo alikuwa Mkristo, lakini baba yake hakuheshimu Biblia. Baba yake alimdokezea jambo katika mazungumzo yao.

"Yakobo, unapaswa kumwoa binti Samueli awe mkeo. Ni msichana mzuri."

Yakobo alishangaa sana, akamwambia, "Baba mimi siwezi kumwoa. Yeye si Mkristo. Biblia inawakataza Wakristo kuonana na wasio Wakristo!"

Baba yake akamwambia, "Mwanangu, Biblia iliandikwa na wanadamu. Hayo ni mawazo ya watu, wala hupaswi kuyafuata."

Je! ungemwambiaje baba yake Yakobo kama ingekuwa ni wewe? Kuna watu wengi kama baba yake Yakobo. Wanafikiri kwamba Biblia ni mawazo na mashauri watu wengine. Pengine



ni kujitenga na uchawi. Hebu tuone yale Biblia inayosema kuhusu Wakristo na uchawi.

MAELEZO

Je! Mungu aliwaambia nini wateule wake kuhusu uchawi? Kumbukumbu la Torati 18:10-12 inatumabia kwamba Mungu aliwaamuru wana wa Israeli wajitenge na uchawi.

Watu tofauti wametajwa kama wabashiri, msihiri, mlogi, mchawi na yule amwombeaye mfu. Watu hawa hujishughulisha na uchawi, na hawampendezi Mungu.

Ni lazima Wakristo wawe safi mbele za Bwana. Kifungu cha 12 kinasema kwamba ye yote anayetenda mambo haya anamchukiza Bwana. Mungu aliwaambia Waisraeli kwamba mataifa wanayoyaendea yafanya mambo haya, lakini wao hawapaswi kufuata mwenendo wao.

Malaika wa Shetani waitwao pepo waliwasumbua watu wakati wa huduma ya Yesu. Katika Marko 5:6-13, mtu mwenye pepo mchafu alimpigia Yesu makelele kwa sauti kuu. Yesu aliyaamuru hao wamtoke. Shetani huwatumia watu kutenda maovu, lakini Kristo ananguvu nyingi kuliko Shetani.

Katika Matendo 8:9-24, tunamwona Petro akimkemea Simoni, mchawi wa Samaria ambaye aliogopewa na watu wengi. Petro alimwambia atubu na aombe msamaha. Petro akamwambia ajitoe kwa Kristo. Petro alimwamini Kristo mtu anapokuwa ndani ya Kristo hapaswi kuwa na hofu ya uchawi.

Katika Matendo 13:6-11, Paulo alikuwa katika kisiwa cha Pafo akiwahubiria watu Neno la Mungu. Lakini Elima, yule mchawi, alijaribu kumshawishi liwali aiache imani hiyo. Paulo alimkemea mtu baada ya kujazwa na Roho Mtakatifu. Akamfanya awe kipofu. Kisha liwali akaamini alipoona

yaliyotendeka. Tunapomwamini Kristo huwa yuko tayari kutusaidia kufanya kazi aliyotupatia.

Katika Matendo 16:16-18, Paulo alikuwa Filipi wakati kijakazi mmoja aliyekuwa na "pepo wa uaguzi" alipomfuata na kumchukiza. Paulo aliamuru pepo huyo amtoke, na akatii. Uwezo wa Mungu ni mkuu kuliko wa Shetani.

Tunaona katika mambo haya yote kwamba Kristo ndiye Mungu mwenye nguvu na uwezo mkuu. Shetani hataweza kamwe kuuzuia uwezo wa Mungu.

**MAFUNZO YA SURA HII KWANGU**

Tunapaswa kuangalia matendo makuu ya Yesu Kristo na vishawishi vya Shetani ambavyo humtatanisha mwanadamu. Tunapaswa kujifunza kutoka kwa watu wengine jinsi ya kuishi maisha ya Kikristo.

Wakristo hawapaswi kuogopa majaribu ya Shetani. Mtu anapojitoa kwa Kristo hapaswi kuogopa uchawi. Hii ni kwa sababu Kristo huwa ngao na nguvu zake.

Biblia inasema, "...yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia" (1 Yohana 4:4). Kila mwamini ana haki ya kudai uwezo mkuu wa Kristo wa kushinda maovu.

Mkristo mwaminifu husimama imara, hata kuwepo uchawi. Wakristo wanapaswa kuvaa silaha za Mungu waweze kupinga hila za Shetani. Soma Waefeso 6:11-17. Sisi wenyewe hatuna silaha wala nguvu za kumpinga Shetani, lakini Mungu ametupa uwezo huu. Je! silaha hizi ni zipi?

Tumeambiwa tujifunge kweli viunoni na kuvaa dirii ya haki kifuani. Tunapaswa kuvaa miguuni mwetu injili ya amani. Ngao ya mwamini ni amani, na chepeo yake ni wokovu. Hizi ndizo sehemu za silaha ambazo zitatulinda kutoka kwa adui. Silaha hizi zitatuwezesha kumshinda Shetani. Lakini tunahitaji



anakupenda jinsi ulivyo. Yesu, Mwana wa Mungu, alifia dhambi zetu ili nasi tuwe wana wa Mungu. Roho Mtakatifu huja kuishi ndani yetu tunapompokea Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wetu. Hatupaswi kuhisi nguvu maalum kabla ya kutujia. Tunaamini na kupokea wajibu wetu ni kumruhusu Roho Mtakatifu atawale na kuongoza maisha yetu anapoingia maishani mwetu. Maisha yasiyo na dhambi ni chombo kisafi cha kutumiwa na Roho Mtakatifu. Hakuna kiwango ambacho Roho Mtakatifu anaweza kufanya kazi maishani mwa mtu, wakati amejitoa kuongozwa na Roho Mtakatifu.

**KAZI YA KUFANYA**

1. Yafikirie maisha yako. Je! umempokea Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wako? Kama bado, unastahili kukata shauri leo?

2. Mwombe Roho Mtakatifu akuonyeshe dhambi zilizoko maishani mwako.

3. Kiri dhambi zote. Soma 1 Yohana 1:9. Mwombe Yesu awe Mwokozi wako.

4. Fikiria sehemu maalum ambazo utahitaji kuongozwa an Roho Mtakatifu. Ombea sehemu hizo.

5. Liambie kanisa lako yale ambayo Yesu anakufanyia maishani mwako.

6. Jadili yale uliyogundua na mshiriki mwingine.

Roho Mtakatifu waliyeahidiwa. Roho Mtakatifu aliwajia wanafunzi siku ya Pentekoste. Roho Mtakatifu ni wa milele na alikuwepo tangu mwanzo. Lakini alikuja kwa njia maalum siku ya Pentekoste kuendelea na kazi ya Mungu duniani.

Tutajifunza aina sita ya kazi ya Roho Mtakatifu.

1. Uumbaji: Roho Mtakatifu ndiye mwenye kupeana uzima. Alikuwepo pamoja na Baba na Mwana wakati wa kuumba ulimwengu. Yungali anafanya kazi ulimwenguni.

2. Kupata Mimba: Roho Mtakatifu ndiye aliyemwezesha Mariamu, mama wa Yesu kupata mimba.

3. Dhihirisha: Roho Mtakatifu hudhihirisha ukweli wa Mungu. Aliwawezesha wanadamu kuandika Maandiko na kutusaidia kuelewa na kufafanua Maandiko.

4. Thibitisho: Roho huukuza ukweli mioyoni mwa wanadamu. Huwashawishi na kuwathibitishia wanadamu ukweli kuhusu Yesu Kristo.

5. Kuongoza: Roho Mtakatifu huwaongoza waamini. Yesu aliahidi kwamba, "Lakini yeye atakapokuja, huyu Roho wa kweli, atawaongosa awatie kwenye kweli yote..." (Yohana 16:13).

6. Kutoa: Roho Mtakatifu huwapa waamini karama tofauti-tofauti.

**MAFUNZO YA SURA HII KWANGU**

Tunapaswa kutambua uhusiano uliopo kati ya Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Umoja wao hauwezi kutenganishwa kamwe. Katika utatu huo tunaye Mungu mmoja ambaye ni mwenye upendo. Mungu kama Baba anampenda mwanadamu na lionyesha upendo wake kwa kumtuma mwanawe Yesu Kristo. _______________(Andika jina lako.) Mungu



silaha ya kujilinda tunapopigana vita na Shetani. Mungu hutupa silaha hii. Hutupatia "...upanga wa Roho ambao ni Neno la Mungu" (Waefeso 6:17). Tunaweza kumvamia na kushinda Shetani tuwapo na Neno la Mungu. Shetani hawezi kamwe kukabiliana nalo.

**KAZI YA KUFANYA**

1. Zungumzia habari za uchawi unapoongea na vijana wengine na uwaelezee yale uliyojifunza katika somo hili.

2. Mwulize rafiki Mkristo akwambie jinsi alivyoona uwezo wa Kristo ukifanya kazi maishani mwake.

3. Soma Kifungu cha Kukumbuka kila asubuhi kabla ya kuanza shughuli zako. Mwombe Mungu akusaidie kuelewa na kukitii.

4. Fikiria akilini mwako jinsi ya kuvaa silaha za Mungu. Vaa kweli na haki jinsi unavyovaa nguo zako. Chukua imani na injili ya amani kama mavazi yako. Jifunike na ufahamu kwamba umeokoka, kisha uchukue ulimwengu. Ongeza sala kwa mavazi yako, jinsi ulivyoagizwa katika Waefeso 6:18. Kisha kabiliana na siku kwa ujasiri wa Yesu Kristo, Bwana wako.

### SURA YA SABA

## ROHO MTAKATIFU NA UTATU

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba Roho Mtakatifu ni sehemu ya utatu wa Mungu.

SOMO KUTOKA: Mathayo 3:13-17

VIFUNGU VYA LEO: Mathayo 3:13-17

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote..." (Yohana 16:13).

## KUSOMA SOMO

### UTANGULIZI

Pengine umewasikia watu wakiwaambia Wakristo kwamba wanaabudu Mungu watatu. Je! huwa tunaabudu Mungu watatu? La, hasha! Maandiko yanatufundisha kwamba kuna Mungu mmoja, Mwenyezi Mungu, Mwumba mbingu na nchi. Tunaamini kwamba Mungu huyu amejifunua kwetu katika utatu. Amejifunua kwetu kama Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Neno utatu, linalotumiwa kueleza jinsi Mungu alivyojifunua kwa mwanadamu, halipatikani katika Biblia. Tunaweza kulielewa vizuri tukijifunza jinsi Mungu alivyojifunua kwetu. Tunaweza kueleza mashaka ya watu kuhusu yale tunayoamini kama tutaelewa mafundisho ya Biblia.

### MAELEZO

Soma Mathayo 3:13-17. Tunaona wazi jinsi Mungu alivyojifunua kama Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Baba alimbariki na kumdhihirisha Mwana wake kwa sauti kuu. Mwana alijitoa akabatizwa, na Roho Mtakatifu alimbariki kwa huduma yake.

Yesu akawaambia, "Mimi na Baba tu umoja" (Yohana 10:30). Ukimwona Yesu umemwona Baba. (Yohana 14:9) Yesu alipowaahidi wanafunzi wake kuja kwa Roho Mtakatifu, aliwaambia "Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele" (Yohana 14:16). Neno hili, Msaidizi mwingine, linamaanisha yule anayefanana na Yesu. Biblia inatumia majina haya, Roho wa Mungu na Roho wa Kristo kumaanisha jambo moja. Hili ni thibitisho lingine la umoja kati ya Baba, Mwana na Roho.



Je! Mungu anawezaje kuwa utatu? Hatuwezi kupata kanuni kama hii katika hesabu zetu. Ni lazima tukubali kwamba hatuwezi kuelewa kabisa hali ya Mungu, lakini Mungu atatusaidia kufahamu ya kutimiza mahitaji yetu. Tutabadilishwa tufanane naye tutakapoenda mbinguni, na tutafahamu mambo yote. Lakini kwa sasa tunaowajibu wa yale tunayofahamu na tuwezayo kufahamu. Baba wazazi hawawezi kuwa mfano kamili jinsi Mungu alivyo Baba yetu. Hata hivyo kuna mambo kadhaa tunayoweza kujifunza kutoka kwao kuhusu Mungu kama Baba. Baba ni watu wanojali, wanaotunza na kuchukua wajibu wa watoto wao. Huwaongoza na kuwaelekeza na kuwapenda. Yesu alimwomba Baba yake. Alimtegemea Mungu kwa mambo yote. Alisema kwamba mambo yote yako mikononi mwa Baba yake. Mungu anatawala kila kitu. Mungu yu macho kila wakati. Halali kamwe. Huchukua wajibu wa baba kwa wale wanaomwendea na kuwafanya watoto wake.

Mwana, Yesu Kristo amewawezesha watu kukutana na Mungu na kuwa wana wa Mungu. (Yohana 1:11-12) Baba alimtuma Mwanawe, Yesu, kuja ulimwenguni na kukutana na mwanadamu. Yesu alizaliwa na mwanamke. Alikuwa Mungu aliyefanyika mwili. (Yohana 1:14) Alitembea, alizungumza na watu na alikabiliana na mateso na hata maajabu ya maisha. Yesu hakufanya dhambi ingawa aliishi kama mwanadamu, lakini alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. Watu wanaweza kushirikiana na Mungu kupitia kwake.

Tunasoma katika Wakolosai 1:19-20 kwamba,"Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae; na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake, akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake...."

Yesu alipaa mbinguni baada ya kufufuka. Kabla ya kuondoka duniani, aliwaambia wanafunzi wake wangojee Yerusalemu